## TAARIFA YA MAELEZO YA CHANJO

# Chanjo ya Homa ya Mafua (Mafua) (Isiyo Hai au Inayoweza Kuunganishwa Tena): *Unachohitaji kujua*

Many Vaccine information Statements are available in Spanish and other languages. See www.immunize.org/vis
Hojas de información sobre vacunas están disponibles en español y en muchos otros idiomas. Visite www.immunize.org/vis

## 1 Kwa nini nipokee chanjo?

Homa ya mafua ("mafua") ni ugonjwa wa kuambukiza unaoenea Marekani kila mwaka, kwa kawaida kati ya mwezi wa Oktoba na Mei.

Mafua husababishwa na virusi vya homa ya mafua, na huenezwa hasa kwa kukohoa, kuchichimua, na uhusiano wa karibu.

Mtu yoyote anaweza kupata mafua. Mafua humshika mtu kwa ghafla na yanaweza kudumu kwa siku kadhaa. Dalili hutofautiana kwa umri, lakini zinaweza kujumuisha:
- homa/baridi
- mwasho wa koo
- maumivu ya misuli
- uchovu
- kukohoa
- maumivu ya kichwa
- makamasi au kuziba pua

Mafua pia yanaweza kusababisha nimonia na maradhi ya damu, na kusababisha kuharisha na kifaa katika watoto. Ikiwa una hali ya kimatibabu, kama vile ugonjwa wa moyo au mapafu, mafua yanaweza kuifanya kuwa mbaya zaidi.

Homa ni hatari zaidi kwa watu fulani. Watoto wachanga na watoto wadogo, watu wenye umri wa miaka 65 na kuendelea, wanawake wajawazito, na watu wenye hali fulani za afya au wenye mfumo dhaifu wa kinga mwilini wako katika hatari kubwa.

Kila mwaka **maelfu ya watu nchini Marekani hufa kutokana na mafua**, na wengi zaidi hulazwa hospitalini.

**Chanjo ya mafua inaweza:**
- kukuzuia kupata mafua,
- kupunguza ukali wa mafua ukiambukizwa, na
- kukuzuia kusambaza mafua kwa familia yako na watu wengine.

## 2 Chanjo za mafua zisizohai na zinazoweza kuunganishwa tena

Dozi ya chanjo ya mafua inapendekezwa kwa kila msimu wa mafua. Watoto wenye umri wa miezi 6 hadi miaka 8 huenda wakahitaji dozi wakati wa msimu sawa wa mafua. Kila mtu mwingine anahitaji dozi moja tu kila msimu wa mafua.

Baadhi ya chanjo ya mafua isiyo hai ina kiasi kidogo sana cha kihifadhi cha zebaki kinachoitwa thimarosali. Utafiti haujaonyesha kwamba thimarosali katika chanjo ni hatari, lakini chanjo za mafua ambazo hazina thimarosali zinapatikana.

Hakuna virusi hai vya mafua katika chanjo za mafua. **Haziwezi kusababisha mafua.**

Kuna virusi vingi vya mafua, na huwa vinabadilika wakati wote. Kila mwaka chanjo mpya ya mafua hutengenezwa kulinda watu kutokana na virusi vitatu au vinne vinavyoweza kusababisha ugonjwa katika msimo wa mafua unaofauta. Lakini hata wakati chanjo hailingani na virusi hivi, bado inaweza kutoa kinga kwa kiasi fulani.

Chanjo ya mafua haiwezi kuzuia:
- mafua yanayosababishwa na kirusi kisichokingwa na chanjo, au
- ugonjwa unaofanana na mafua lakini sio mafua.

Huchukua takriban wiki 2 kwa kinga kuundwa mwilini baada ya kupokea chanjo, na kinga hudumu katika msimu mzima wa mafua.

## 3 Baadhi ya watu hawafai kupokea chanjo hii

Mjulishe mtu anayekupa chanjo:
- **Ikiwa una mizio yoyote mikali ya kutishia maisha.** Ikiwa ushawahi kuwa na mzio wa kutishia maisha baada ya dozi ya chanjo ya mafua, au unapata mzio mkali katika sehemu yoyote ya chanjo hii, huenda ushauriwe usipokee chanjo hiyo. Aina nyingi, lakini sio zote, za chanjo ya mafua zina kiasi kidogo cha protini ya yai.
- **Ikiwa una Guillain-Barré Syndrome (pia inayojulikana kama GBS).** Baadhi ya watu wenye historia ya GBS hawafai kupokea chanjo hii. Jambo hili linafaa kujadiliwa na daktari wako.
- **Ikiwa huli vizuri.** Kwa kawaida huwa ni sawa kupokea chanjo ya mafua wakati wewe ni mgonjwa kidogo, lakini unaweza kuambiwa urudi unapopata nafuu.

## 4 Hatari za mzio wa chanjo

Ukitumia dawa zozote, hata chanjo, huwa kuna uwezekano wa madhara. Madhara haya huwa kidogo na hupotea yenyewe, lakini mizio mikali pia inawezekana.

Watu wengi wanaopata sindano ya homa huwa hawapati matatizo yoyote nayo.



U.S. Department of Health and Human Services
Centers for Disease Control and Prevention

**Matatizo yasiyo hatari** baada ya kupokea sindani ya mafua yanajumuisha:
- maumivu, wekundu, au uvimbe kwenye sehemu iliyodungwa sindano
- sauti nzito
- mwasho, wekundu kwenye macho
- kukohoa
- homa
- maumivu
- maumivu ya kichwa
- mwasho
- uchovu

Ikiwa matatizo haya yatatokea, huanza mara tu baaada ya kupokea sindano na huchukua siku 1 au 2.

**Matatizo hatari zaidi** baada ya kupokea chanjo ya mafua yanaweza kujumuisha mambo yanayofuata:
- Huenda kukawa na ongezeko la hatari kiasi ya Guillain-Barré Syndrome (GBS) badaa ya kupokea chanjo ya mafua isiyo hai. Hatari hii imekadiriwa katika kesi 1 au 2 zaidi kwa kila watu milioni moja wanaopokea chanjo. Kiwango hiki kiko chini sana kuliko hatari ya matatizo makali kutoka kwa mafua, yanayoweza kuzuiwa na chanjo ya mafua.
- Watoto wachanga wanaopokea chanjo ya mafua pamoja na chanjo ya nimonia (PCV13) na/au chanjo ya DTaP kwa wakati mmoja wana uwezekano mkubwa wa kupata kifafa kinachosababishwa na homa. Muombe daktari wako maelezo zaidi. Mwambie daktari wako kama mtoto anayepokea chanjo ya mafua ashawahi kupata kifafa.

**Matatizo yanayoweza kutokea baada ya kudungwa chanjo yoyote:**
- Wakati mwingine watu huzimia baada ya utaratibu wa matibabu, ikiwa ni pamoja na chanjo. Kuketi au kulala chini kwa takriban dakika 15 kunaweza kusaidia kuzuia kuzirai, na majeraha yanayosababishwa na kuanguka. Mwambie daktari wako ikiwa unahisi kizunguzungu, au kubadilika kwa namna unavyoona au kelele katika masikio.
- Watu wengine hupata maumivu makali mabegani na huwa na ugumu wa kusongeza mkono mahali ambapo sindano ilidungwa. Jambo hili hufanyika mara chache sana.
- Dawa zozote zinaweza kusababisha mzio mkali. Mizio kama hii kutoka kwa chanjo huwa nadra sana, inakadiriowa takriban dozi 1 kati ya dozi milioni moja, na inaweza kutokea ndani ya dakika chache hadi saa chache baada ya chanjo.

Kama tu dawa zozote, kuna nafasi ndogo sana ya chanjo kusababisha majeraha makali au kifo.

Usalama wa chanjo hufuatiliwa wakati wote. Kwa maelezo zaidi, tembelea: **www.cdc.gov/vaccinesafety/**

## 5 Na kukiwa na mzio hatari?

**Ninafaa kutafuta nini?**
- Tafuta kitu chochote kinachokutia wasiwasi, kama vile dalili za mzio mkali, homa kali sana, au tabia isiyo ya kawaida.

  Dalili za mzio mkali zinaweza kujumuisha mabaka ngozini, uvimbe usoni na kwenye koo, ugumu wa kupumua, mapigo ya kasi ya moyo, kizunguzungu, na udhaifu. Dalili hizi huanza baada ya dakika chache hadi saa chache baada ya chanjo.

**Ninafaa kufanya nini?**
- Ikiwa unafikiria ni mzio mkali au jambo lingine la dharura ambalo haliwezi kusubiri, piga simu kwa 9-1-1 na umpeleke mtu katika hospitali iliyo karibu nawe. La sivyo, mpigie daktari wako simu.
- Mzio unafaa kuripotiwa kwa Mfumo wa Kuripoti Matukio Mabaya ya Chanjo (VAERS). Daktari wako anafaa kutoa ripoti hii, au unaweza kufanya hivyo mwenyewe kupitia tovuti ya VAERS katika **www.vaers.hhs.gov**, au kwa kupiga simu kwa **1-800-822-7967**.

*VAERS huwa haitoi ushauri wa kimatibabu.*

## 6 Programu ya Fidia ya Majeraha ya Chanjo ya Kitaifa

Programu ya Fidia ya Majeraha ya Chanjo ya Kitaifa (VICP) ni programu ya shirikisho iliyoundwa kuwafidia watu ambao huenda wakawa wamejeruhiwa na chanjo fulani.

Watu wanaoamini wamejeruhiswa na chanjo wanaweza kupata maelezo kuhusu programu hii na kuhusu kuripoti madai kwa kupiga simu kwa **1-800-338-2382** au kutembelea tovuti ya VICP katika **www.hrsa.gov/vaccinecompensation**. Kuna kikomo cha muda wa kuripoti madai ya fidia.

## 7 Ninaweza kupata maelezo zaidiaje?

- Muulize mtoa huduma wako wa afya. Anaweza kukupatia kupeperushi furushi la chanjo au kupendekeza vyanzo vingine vya maelezo.
- Piga simu kwa idara ya afya iliyo karibu na wewe au ya jimbo.
- Wasiliana na Vituo vya Udhibiti na Uzuiaji wa Magonjwa (CDC):
  - Piga simu kwa **1-800-232-4636** (**1-800-CDC-INFO**) au
  - Tembelea tovuti ya CDC katika **www.cdc.gov/flu**

Vaccine Information Statement
Inactivated Influenza Vaccine - Kiswahili
08/07/2015
Office Use Only
42 U.S.C. § 300aa-26
Translation provided by Minnesota Department of Health